
# Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
# Taarifa ya Robo mwaka, Robo ya Pili, 2024

MUUNGANO WA VIONGOZI WA AFRIKA KATIKA UDHIBITI WA MALARIA

ALMA

## Kadi ya Alama ya Tathmini na Uwajibikaji




**Vipimo**

| | |
|---|---|
| **Kugharamia** | |
| Makisio ya fedha za ununuzi wa Vyandarua na Viuatilifu Ukoko kwa kipindi cha (2024-2026) (% ya mahitaji) | 97 |
| Sekta ya Umma kugharamia Dawa Mseto na Vitendanishi kwa kipindi cha (2024-2026)(% ya mahitaji) | 100 |
| % ya fedha zilizotengwa kutekeleza Mpango Mkakati wa Malaria kwa kipindi (2024-2026) | 78 |
| **Sera** | |
| Kusaini, Kuidhinisha na kuwasilisha Mkataba wa AMA AUC | |
| Uwepo wa Mikakati inayolega kambi za wakimbizi kwenye mpango mkakati wa malaria | |
| Uwepo Uwepo wa Mikakati inayolega watu wa ndani ya nchi wasio na makazi maalum kwenye mpango mkakati wa malaria | |
| Nchi inatoa taarifa za uzinduzi wa Kampeni ya Ziro Malaria Inaanza na mimi | |
| Nchi inatoa taarifa za uzinduzi wa Kampeni ya Ziro Malaria Inaanza na mimi | |
| **Ufuatiliaji wa Usugu, Utekelezaji na Matokeo yake** | |
| Tafiti za kufuatilia ufanisi wa dawa za kutibu malaria umefanyika tangu mwaka 2019 na taarifa zake kutumwa Shirika la Afya Duniani | |
| Aina ya makundi yaliyothibitishwa kujenga kukabiliwa na usugu dhidi ya mbu kwenye vituo maalum vya ufuatiliaje (Sentinel Sites) | |
| Ufuatiliaji wa usugu wa mbu dhidi ya viuatilifu tangu 2015 na taarifa kuripotiwa kwa Shirika la Afya Duniani | |
| Akiba ya vitendanishi (RDTs) (Ya zaidi ya miezi 6) | |
| Akiba ya dawa mseto (ACTs) (Ya zaidi ya miezi 6) | |
| Kampeni ya vyandarua vyenye dawa ya muda mrefu/unyunyuziaji wa dawa ya ukoko (LLINS/IRS) inaenda kwa mujibu na malengo | |
| Kampeni ya vyandarua vyenye dawa ya muda mrefu/unyunyuziaji wa dawa ya ukoko (LLINS/IRS) inaenda kwa mujibu na malengo | 82 |
| Kupungua kwa Idadi ya Visa vipya kwa asilimia 55 au zaidi kwa mwaka 2022 (ukilinganisha na takwimu za 2015) | |
| Kupungua kwa idadi ya vifo kwa asilimia 55 au zaidi kwa mwaka 2022 (ukilinganisha na takwimu za mwaka 2015) | |
| **Viashiria vya Afya ya uzazi, afya ya mtoto na UVIKO 19** | |
| Idadi waliofikiwa na umezezeshaji wa dawa za kinga tiba dhidi Magonjwa ya Tropiki yaliyosahaulika kwenye jamii (NTD index, %)(2022) | |
| % ya ugawaji dawa kwa walengwa ili kufikia Malengo ya Shirika la Afya Duniani | 75 |
| Makadirio ya asilimia ya watoto, kati ya miaka 0-14, waishio na VVU ambao wanapata dawa za ARV (2023) | 66 |
| Kiwango cha Utoaji wa dozi mbili za vitamin A katika 2022 | 90 |
| Kiwango cha chanjo ya DPT3 2023 (miongoni mwa watoto wenye miezi 0-11) | 93 |

Maambukizi ya Malaria yameenea karibu sehemu zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuwepo kwa viwango vya juu katika msimu.

Taarifa ya utekelezaji ya mwaka 2022, inaonesha idadi ya wagonjwa wa Malaria ilikuwa 3,666,741 na jumla ya vifo 1,538 vilitokea kutokana na malaria.

**Ufunguo**

- Lengo limefikiwa/utekelezaji unaendelea
- JUhudi zaidi zinahitajika kufikia lengo
- Utekelezaji upo nje ya lengo
- Hamna Takwimu
- Haihusiki

| | |
|---|---|
| **Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ripoti ya ALMA, Robo ya Pili, 2024.** | MUUNGANO WA VIONGOZI WA AFRIKA KATIKA UDHIBITI WA MALARIA ALMA |

## Malaria

Bara la Afrika ndio kitovu cha kuonesha madhara ya dhoruba kali yanayotokana na tishio la kuvuruga utoaji huduma za Malaria na kuathiri maendeleo yaliyopatikana katika udhibiti wa Malaria kwa miongo kadhaa iliyopita. Hivyo tunalazimika kuchukua hatua za haraka ili kuzuia na kupunguza hali mbaya kufuatia msukosuko wa kifedha unaoendelea duniani, kuongezeka kwa tishio la kibailojia, mabadiliko ya hali ya hewa na migogoro ya kibinadamu. Vitisho hivi vinawakilisha dharura mbaya zaidi inayozikabili nchi na kutishia mafanikio yaliyopatikana katika udhibiti wa Malaria kwa takriban miaka 20, na huenda litasababisha Malaria kuongozeka na milipuko ya magonjwa iwapo hayatashughulikiwa. Nchi wanachama wa Umoja wa Afrika ina pengo la takriban dola za marekani bilioni 1.5 ili kuendeleza huduma zilizopo ambazo bado hazitoshelezi mahitaji katika udhibiti wa Malaria kati ya sasa hadi ifikapo mwaka 2026. Ili kurejea katika mwenendo sahihi kuelekea kutokomeza Malaria, tunahitaji kuhamasisha kupata fedha nyingine kiasi cha dola za marekani bilioni 5.2 kila mwaka, ili kufadhili kikamilifu utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Malaria.

Mabadiliko ya hali ya hewa ni moja ya tishio kubwa katika utekelezaji uliofanyika mpaka sasa. Afrika inakumbwa na hatari inayotokana na mabadiliko ya hali ya hewa, na ifikapo mwaka 2030, zaidi ya watu milioni 150 watakuwa katika hatari ya kupata maambukizi ya Malaria kutokana na hali ya hewa ya joto na kuongezeka kwa mvua. Majanga yanayotokana na mabadiliko ya hali ya hewa yatawafanya mamilioni ya watu kuhama maeneo yao na kuharibu miundo mbinu ya barabara, vituo vya huduma na changamoto ya upatikanaji wa huduma za afya. Kuna uharaka wa kuondoa kaboni na kupunguza alama ya kaboni. Ni lazima kutekeleza ufumbuzi jumuishi na kushirikisha Sekta mbalimbali ili kupata majawabu sahihi kwa changamoto zilizopo, na kurekebisha mifumo ya afya ili kukabiliana na tishio la mabadiliko ya hali ya hewa na magonjwa ya mlipuko. Ni lazima pia kuchukua hatua kushughulikia tishio la usugu wa viuatilifu na dawa za kutibu Malaria, kupungua ufanisi wa vipimo vya haraka vya uchunguzi wa Malaria, na kuwepo kwa mbu aina ya *Anofelesi stephensi* ambae anaeneza Malaria kwa maeneo yote - Mjini na Vijijini. Habari njema ni kuendelea kuboreshwa na kuongezeka kwa seti ya zana mbalimbali mpya za kudhibiti Malaria.

Shirika la Afya Duniani limethibitisha matumizi ya vyandarua venye viuatilifu makundi mawili ambavyo vina ufanisi mkubwa kwa zaidi ya asilimia 43, ukilinganisha na vyandarua vya kawaida. Matumizi ya vyandarua vyenye ufanisi zaidi vitasaidia kushughulikia athari zitokanazo na usugu. Aidha, dawa mpya za kutibu malaria na chanjo aina mbili za malaria kwa watoto tayari zimepitishwa kwa matumizi na nchi kadhaa za Afrika zimeanza kutumia zana hizo mpya za udhibiti wa Malaria. Kuongezwa kwa afua hizi kutasaidia kufikia lengo la kutokomeza kabisa Malaria. Hili litahitaji mbinu jumuishi, na Malaria ikitumika kuonesha njia ya kujiandaa kukabiliana na milipuko ya magonjwa, mabadiliko ya hali ya hewa, utoaji huduma za afya ya msingi, na kuwafikia wananchi wote wenye uhitaji katika utoaji wa huduma. Ni lazima kufanya kazi kwa juhudi ili kuendeleza na kuongeza uhamasishaji wa rasilimali fedha kutoka vyanzo vya ndani, ikijumuisha mabaraza na mfuko wa udhibiti

wa Malaria na magonjwa yasiyopewa kipaumbele ambazo wamekusanya fedha zaidi ya dola za marekani milioni 60.

## Hatua iliyofikiwa katika Utekelezaji.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imepata uhakika wa rasilimali fedha kwa ajili ya kuendeleza mikakati ya ugawaji wa vyandarua, ununuzi wa dawa mseto na vitendanishi kwa kipindi chote cha miaka mitatu ya granti 2024-26. Aidha imeendelea kufuatilia taarifa ya makundi ya viuatilifu ambayo yameonesha usugu kwa mbu waenezao Malaria tangu mwaka 2015, na kila mwaka nchi imekuwa ikitoa taarifa ya usugu huo kwa Shirika la Afya Duniani. Kutokana na ufuatiliaji huo, taarifa ya usugu imesaidia kufanya maamuzi ya matumizi ya vyandarua venye ubora na ufanisi zaidi.

Tanzania imeendelea na utaratibu wa kupima na kufuatilia ufanisi wa dawa za kutibu Malaria, toka mwaka 2018 ili kugundua uwepo wa usugu mapema, na kutoa taarifa ya ufuatiliaji huo kwa Shirika la Afya Duniani. Mpango Mkakati wa kudhibiti Malaria, umejumuisha shughuli mbalimbali zinazolenga pia kuwafikia wakimbizi. Aidha imeonesha uongozi katika kudhibiti Malaria kupitia ushiriki wake kwenye Mpango maalum kwa nchi zilizo na maambukizi makubwa ya Malaria duniani, na hivi karibuni, ilitia saini Tamko la Yaunde. Tanzania tayari ilishazindua Kampeni ya Ziro Malaria Inaanza na Mimi.

Sambamba na vipaumbele kama Ajenda ilivyowasilishwa na Mwenyekiti wa ALMA, Mhe. Umaro Sissoco Embaló, Rais wa Jamhuri ya Guinea Bissau, Tanzania imeboresha mbinu za ufuatiliaji na taratibu za uwajibikaji katika kutekeleza mikakati ya udhibiti wa Malaria, na kuanzisha matumizi ya Kadi ya Alama ya Tathmini na Uwajibikaji kuelekea kutokomeza kabisa Malaria nchini, pamoja na kuwa bado Taarifa za Kadi hazijaunganishwa katika Habu. Tanzania imeshazindua Baraza na Mfuko wa Kutokomeza Malaria.

## Matokeo.

Taarifa ya utekelezaji ya mwaka 2022, inaonesha idadi ya wagonjwa wa Malaria ilikuwa 3,666,741 na jumla ya vifo 1,538 vilitokana na Malaria.

## Changamoto kuu ni:

- Kuhakikisha tunaendelea kutoa kipaumbele na kutenga fedha kwa ajili ya Zanzibar, hasa ikizingatiwa kuwa maambukizi ya Malaria visiwani humo yanaendelea kupungua.
- Kushughulikia upungufu wa rasilimali fedha ili kuweza kutekeleza kikamilifu na kwa ufanisi Mpango Mkakati wa Malaria nchini.
- Kushughulikia Tishio la uwepo wa usugu wa viuatilifu na dawa za kutibu Malaria.

## Utekelezaji wa Mapendekezo Yaliyopita.

| Lengo | Vipengele vya Utekelezaji | Muda wa Kukamilisha Utekelezaji | Hatua ya Utekelezaji | Ufafanuzi wa shughuli/ mafanikio ukilinganisha na taarifa ya utekelezaji wa robo iliyotangulia. |
|---|---|---|---|---|
| Uhamasishaji katika kupata Rasilimali. | Kazi ya kutafuta rasilimali fedha ili kuziba mapengo muhimu katika ufadhili wa Malaria. | Robo ya 4 2024. | | Tanzania imeweka kipaumbele kwa afua, kulingana na utabaka wa kitaifa ili kuongeza athari, na kulenga kuzuia Malaria kwa kutumia vyandarua venye dawa katika maeneo ya vijijini ambayo yana maambukizi makubwa na ya wastani ya Malaria. Mahitaji kwa ajili ya matibabu yanashughulikiwa, hata hivyo, rasilimali hazipatikani katika kushughulikia suala la usugu wa vimelea kwa dawa za kutibu Malaria. Baraza na Mfuko wa Kutokomeza Malaria lilizinduliwa hivi karibuni, linafanyia kazi ya uhamasishaji wa rasilimali kwa kushirikiana na Mpango wa Taifa wa kudhibiti Malaria, ili kuweka kipaumbele kwa mapungufu katika maeneo muhimu kwa uhamasishaji wa rasilimali.<br><br>Hii ni pamoja na kuimarisha ushirikiano wa Sekta mbalimbali kati ya sekta zote za serikali zenye maeneo muhimu yaliyotambuliwa na kuelekezwa kwa Wizara zote. Hivi karibuni Serikali imefanya kazi ya ziada kupata rasilimali ili kusaidia udhibiti wa viluilui wa mbu katika mazalia.<br><br>Rasilimali zinapatikana kupitia ufadhili wa Mfuko wa Rais wa Marekani wa Kushughulikia Malaria – PMI, katika kusaidia mafunzo ya ufanisi wa tiba katika maeneo yenye mambukizi ya wastani hadi maambukizi ya juu ya Malaria. Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria umeanzisha kikosi kazi cha kukagua matokeo ya tafiti za ufanisi ili kusaidia katika kuendeleza na kuchukua hatua ya kukabiliana na usugu kulingana na muktadha wa eneo husika. |
| Matokeo | Kazi ya kutengeneza Mpango wa utekelezaji ili kusaidia utekelezaji wa Tamko la Yaunde. | Robo ya 4, 2024 | | Tanzania imepiga hatua katika utekelezaji wa Tamko la Yaunde. Kwa mfano Baraza na Mfuko wa Kutokomeza Malaria imeitisha mkutano na viongozi wa dini ili kuhamasisha jamii na makampuni ya uchimbaji madini kutoa fedha zaidi kwa ajili ya udhibiti wa Malaria. Aidha imeitisha Mkutano wa Makatibu Wakuu wa Wizara ili kuhimiza Ufadhili na Ushirikiano wa Sekta mbalimbali. Usimamizi wa matibabu ya Malaria ngazi ya jamii inaendelea katika maeneo yasiyopata huduma. |

## Huduma ya Afya ya Uzazi kwa Mama, Watoto, Wachanga na Vijana.

### Hatua iliyofikiwa.

Tanzania imefanikiwa sana na kufikia kiwango cha juu katika kiashiria cha ugawaji wa vidonge vya Vitamin A na Chanjo ya DPT3. Tanzania imeandaa utaratibu makini wa kusimamia na kufuatilia utekelezaji, pamoja na Kuzindua Kadi ya Alama ya Tathmini na Uwajibikaji kwa huduma ya Afya ya Uzazi kwa mama, watoto, wachanga, na vijana, pamoja na ushirikishaji wa wadau katika eneo la lishe.

## Magonjwa ambayo yalikuwa hayapewi Kipaumbele.

### Hatua iliyofikiwa:

Mafanikio ya utekelezaji wa mikakati kwa magonjwa ambayo yalikuwa hayapewi kipaumbele hapa nchini Tanzania, yanapimwa kwa kutumia thamani ya kielezo kinachozingatia kiwango cha utekelezaji wa tiba-kinga kwa magonjwa ya matende, usubi, kichocho na trakoma.

Kwa mwaka 2022, kiwango cha utekelezaji wa tiba-kinga kilikuwa asilimia 38 katika udhibiti wa kichocho, asilimia 78 kwa usubi, asilimia 84 kwa matende na asilimia 86 kwa trakoma. Kwa ujumla kiwango cha utekelezaji kwa magonjwa yasiyopewa kipaumbele kwa Tanzania kwa mwaka 2022 ni alama 68, ikiwa ni ongezeko kubwa ukilinganisha na kiwango cha mwaka 2021 ambapo thamani ya kielezo ilikuwa alama 63 tu.

Tanzania imefikia Malengo ya Shirika la Afya ya Dunia katika ugawaji wa dawa kinga za matende na trakoma. Nchi imeimarisha sana mbinu za ufuatiliaji na uwajibikaji ikijumuisha kuandaa Kadi ya Alama ya Tathmini na Uwajibikaji kwa magonjwa ambayo yalikuwa hayapewi kipaumbele.

Aidha Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tayari imeshasaini Tamko la Kigali.